KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 15, Issue 2

16th Dhul Qa'dah 1432

14th Oct, 2011

YALIYOMO

AL-MAHDI 1 - 4

AL-MAHDI, MUHAMMAD BIN ABDULLAAH

Na: Sheikh A. Hijazi (حفظه الله)

Kila aliyetunukiwa na ufahamu timamu anajua yakwamba huyo Mahdi ambaye anyengojewa na ma-Shi'ah, hayupo na wala hakuwepo. Taifa la Uislamu limepambana na matatizo chungu nzima na maafa kwa sababu ya Imani hii ya kutatanisha iliyobletwa na ma-Shi'ah na kusambazwa kumuhusu Mahdi.

Katika mfumo wa ki-Shi'ah, kuwaamini ma-Imaam ndio msingi wa Imani yao. Hatahivyo, mfumo kama huo unafanana na mifumo ya wa-Giriki na wa-Pashya, na pia ni kama imani za Mataifa mengine ya *ki-Jaahiliyyah.*

Ma-Sunni wanaamini yakwamba al-Mahdi atakuwa ni mtu wa kawaida, atakaezaliwa na mwanamke wa kawaida, atalelewa na watu wa kawaida na kuishi maisha ya kawaida pamoja na watu wa zama zake. Hatoishi kwenye mapango, kama wanavyoamini ma-Shi'ah. Wao wanamsubiri Mahdi wao ajitokeze kutoka kwenye pango linalodaiwa, ambamo wanadai yakwamba amekuwepo mafichoni humo kwa takriban zaidi ya karne kumi.

Kwa hakika, al-Mahdi atakuwa ni Imaam na vilevile atakuwa ni Khalifa, miongoni mwa ma-Khalifa wengine waliowahi kuwatawala Waislamu kwa uadilifu. Lakini hatahivyo, jambo la kumtafautisha al-Mahdi na ma-Khalifa wengine ni kwamba atakutana na 'Issa, mwana wa Maryam (عليه السلام).

Vilevile, 'Issa (عليه السلام) ataswali nyuma ya al-Mahdi. Allaah atampa al-Mahdi uwezo wa kutawala taifa la Waislamu kwa uadilifu kwa muda wa usiku mmoja. Ataeneza uadilifu katika ulimwengu mzima, kama ilivyoenezwa dhulma. Ataongoza taifa la ki-Islamu kunako ukombozi wa pili wa Constantinople na hata Rome.

KHALIFA ANAEFUATA UONGOFU WA MTUME (صلى الله عليه وسلم)

Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) ameeleza yakwamba muda mfupi kabla ya mwisho wa ulimwengu, taifa la Uislamu litaongozwa na Khalifa ambaye atakaefuata uongofu ulioletwa pamoja na Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Amepokea Hudhaifah bin al-Yamani yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم), *"Utume (kumaanisha yeye mwenyewe) utabaki na nyinyi kwa muda apendao Allaah ubakie, kisha Allaah atauinua pindi atakapopenda kuuinua. Baada ya hapo, kutakuwa na u-Khalifa utakaofuata uongofu wa Utume utakaobaki nanyi kwa muda apendao Allaah ubakie nanyi. Kisha atauinua pindi atakapopenda kuuinua. Na baada ya hapo, kutakuwa na utawala wa mabavu na dhulma* [utawala wa wafalme wa ki-Islamu wenye dhulma za kiasi fulani]*, na utabaki nanyi kwa muda apendao Allaah ubaki nanyi. Kisha, kutakuwa na utawala wa maonevu (ki-Dikteta), na utabaki nanyi kwa muda apendao Allaah ubaki nanyi. Kisha, Allaah atauondoa pindi apendapo kuuondoa. Kisha kutakuwa na u-Khalifa utakaofuata uongofu wa Utume."*

Kisha akasema Hudhaifah, "Mtume (صلى الله عليه وسلم) akanyamaza kusema." [al-Silsilah as-Swahihah, vol.1, no.5]. Sababu ya kuitaja hadeeth hii hapa ni kueleza yakwamba al-Mahdi atakuja kuishi

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

THE QUR'AN & SUNNAH HAJJ / 'UMRAH AGENCY

1432HIJRI/ 2011 C.E

Assalaamu 'Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:
Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah mwaka huu 1432 Hijri/ 2011, tumeanza Barnaamij ya kupeleka watu Hajj.

Mipangilio Ya Safari

- Kuondoka ni katika wiki ya mwisho ya mwezi wa Dhul Qa'dah
- Kurudi ni mwisho wa mwezi wa Dhul-Hijjah
- Safari itaanza Mombasa – Nairobi – Jeddah
- Kurudi ni Jeddah – Nairobi – Mombasa
- Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli, Usafiri na Chakula – mara 3 kwa siku tukiwa Mina kwa siku tano)
- Class "B" ni $3800 U.S Dollars / Class "C" ni $3200 U.S Dollars
- Amma mas'ala ya Chakula (Makka na Madinah) kila mtu ni juu yake
- Tutakuwa na Darsa juu ya mas'ala ya Hajj kabla ya kuondoka na tutakapokuwa Makkah
- Tutaandamana na Daktari wetu kutoka hapa Mombasa Insha Allaah

Kwa Maelezo Zaidi

Fika katika Maktaba ya QSS iliyoko ubavuni mwa Tajj Hotel (Duka la tatu baada ya Duka la vitabu vya Dini), au
Wasiliana nasi kwa kutuandikia barua Pepe kwa info@qssea.net, au
Tupigie simu nambari mojawapo ya hizi zifuatazo:
+254 723471820 au +254 721473181, au +254 700365253

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

katika zama za mwisho za ma-Khalifa waongofu alizozitaja Mtume (صلى الله عليه وسلم). Katika hadeeth hii, Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliigawanya tareekh ya taifa la Uislamu kwenye daraja zifuatazo:

1. Enzi za Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم).
2. Ukhalifa wenye kuhukumu kulingana na uongofu ulioteremshwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Enzi hizi zimeitwa kwa jina la "Enzi Za Makhalifa Waongofu", kuanzia kwa Abu Bakr, kisha 'Umar, kisha 'Uthman na kumalizikia kwa mauaji ya 'Ali Bin Abi Twaalib (رضي الله عنهم). Baadhi ya wanavyuoni wameongezea zama fupi za al-Hasan Bin Ali, mjukuu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Haya ndiyo miaka thalathini aliyoitaja Mtume (صلى الله عليه وسلم) ambayo ndani yake kulikuwemo utawala wa Makhalifa waongofu. Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Ukhalifa utabaki katika taifa langu baada ya kuondoka mimi kwa miaka thalathini. Kisha utafuata ufalme baada ya hapo."* [Ahmad, at-Tirmidhee na wengineo, *swaheeh ul Jaami' as-Swagheer*, no. 3341].
3. Utawala wa mabavu usiokuwa na uadilifu. Utawala huu utakuwa na dhulma kwa daraja zenye kutafautiana baina ya mfalme mmoja hadi mwengine. Zama hizi zilianza baada ya al-Hasan Bin Ali mpaka zikaingiana na zama za *Umayyad*, *Abbasid*, *Mamluk* na mpaka kuanguka kwa utawala wa *Uthmaaniyyah* katika karne ya Ishirini. Muda huu umehusisha Mataifa yote yaliyotawala katika ulimwengu wa Uislamu kwenye karne hizo. Lakini hatahivyo, tumeweka kando utawala wa wale viongozi ambao uongozi wao ulifanana na uongozi wa Makhalifa waongofu, kama vile utawala wa Abdullaah Bin az-Zubayr na Umar Bin Abdul-Aziz. Hawa wawili wamezingatiwa kuwa ni miongoni mwa Makhalifa waadilifu kutokana na kabila la ma-Quraysh waliotawala au watakaotawala Taifa la Uislamu.
4. Utawala wa ki-dhalimu. Muda huu ulianza mwishoni mwa utawala wa Uthmaaniyyah na kuendelea mpaka hivi sasa. Twamuomba Allaah atuokoe kutokamana na maovu na dhulma za zama hizi na kwamba tushuhudie mwisho wake hivi karibuni. Zama hizi zinakusanya mifumo ya uongozi yenye kutawala Ulimwengu wa ki-Islamu, emma ikiwa ni Ufalme wa kibeberu, siyasa za ki-Mashariki, mataifa yenye kuendeshwa na makafiri, kama yale baada ya vita vya Kwanza vikuu vya Ulimwengu, serikali zenye kujali maoni na fikra za watu au serikali inayofuata sera ya Jamuhuri, ambazo zote hizo ni zenye kutafuta kumnyang'anya Allaah haki Yake kama Mtunga sheriya wa Kipekee wa kila jambo la Maisha na Dini. Pindi Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipotaja zama za Ummah huu zitakavyokuwa, aliziorodhesha kulingana na sampuli ya Taifa lenyewe, emma taifa lenye kudhulumu, au lenye kufuata uongofu wa Mtume, au Udikteta na Ubepari, kama tuonavyo siku hizi.
5. Kuregea kwa Ukhalifa unaotawala kulingana na uongofu wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Muda huu unahitaji Waislamu wajitayarishe na kujitahidi kuja kwake kusikokuwa na shaka, kwa kuisambaza 'Ilmu ya Kitaab na Sunnah kulingana na ufahamu wa wema waliotutangulia, *as-Salaf us Swaalih.* Hii ni kwa sababu hakuna kiwezacho kuhuisha Taifa hili isipokuwa kile kilichowahuisha waliowatangulia. Mpaka zama hizi za mwisho zitakapofika, dini itakuwa ni geni, kama ilivyoanza ilipokuwa Makkah, ilikuwa ni geni kwa mabwana zake na watumwa wake, wenye nguvu na wanyonge, wanawake wao na watoto wao. Wale watakaong'ang'ana katika kuimarisha zama hizo za uadilifu ndio hao *al-ghurabaa*, wageni kama alivyowaita Mtume (صلى الله عليه وسلم), ambao ndio watakaoibeba dini hii kwa 'Ilmu, ufahamu wenye muelekeo na uthabiti wa moyo. Watajitolea nafsi zao bila ya kulazimishwa, wapambane na misukosuko, na kuteswa, kwa kusubiri na kuwa na msimamo. Wao watafuata naseeha za Mtume (صلى الله عليه وسلم) pindi aliposema: *"Kwahivyo, shikamaneni na Sunnah zangu na Sunnah za Makhalifa waongofu, zishikeni (ziumeni) kwa meno yenu! Na mujitahadhari na mambo ya uzushi (kwenye dini), kwani kila lenye kuzuliwa ni bid'ah, na kila bid'ah ni upotofu, na kila upotofu mwisho wake ni motoni."* [*Swaheeh ul Jaami' as-Swagheer*, no. 2549].

Hao *ghurabaa* ndiwo ambao, Insha-Allaah, watakaorekebisha yale ambayo watu waliyoyageuza na kuyabadilisha katika Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) baada ya kuondoka kwake ulimwenguni. Watapigana vita kwa ajili ya Allaah na wawashinde wapinzani wao. Hawatolegeza ukali wao hata wakiwa mbele ya nyuso za waliowahama na kuwakataa, mpaka Allaah atakapoleta Hukmu Yake (Kiyama), haliyakuwa wao wameshikilia imara juu ya njia yake. Twamuomba Allaah (سبحانه وتعالى) atuja'alie kuwa thabiti juu ya njia ya Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) na njia iliyoandamwa na Maswahaba na wale waliofuata uongofu wao mpaka siku ya Malipo.

AHAADEETH ZINAZOMUHUSU *AL-MAHDI* NA ALAMA ZA KUONYESHA YAKWAMBA YEYE YUKO JUU YA UONGOFU

Kuna ahaadeeth nyingi kumuhusu al-Mahdi. Baadhi yake ni dha'eef, lakini watu wamezishikilia mno. Lakini hatahivyo, kuna ahaadeeth nyingi pia ambazo ni swaheeh, na baadhi nyengine ni *hasan* (zinazokubalika) na baadhi nyengine ni swaheeh kama walivyokubaliana wanavyuoni wa hadeeth.

Zifuatazo ni baadhi ya ahaadeeth zenyewe kumuhusu al-Mahdi. Umm Salamah, mkewe Mtume (صلى الله عليه وسلم) amehadithia yakwamba, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"al-Mahdi atatokamana katika jamii yangu, katika kizazi cha Faatimah."* [Abu Daawud, Ibn Maajah na al-Haakim, Swaheeh Sunan Abu Daawud, no. 3603].

Vilevile, Ibn Mas'ud amepokea yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Hata ikibaki siku moja katika maisha haya, basi Allaah atairefusha siku hiyo mpaka mtu, kutoka katika kizazi changu atakapokuja. Jina lake litakuwa ni kama jina langu na jina la babake litakuwa ni kama jina la babangu. Ataeneza uadilifu na usawa baada ya kuwa na dhulma na maonevu."* Vilevile, Ali Bin Abi Twaalib amepokea yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Lau kutabaki hata siku moja ya maisha ya hapa ulimwenguni, hapo Allaah atamuinua mtu anaetokana na kizazi changu atakaeujaza (ulimwengu) uadilifu baada ya kujaa dhulma nyingi."* Ahmad, Abu Daawud na at-Tirmidhee wamepokea yakwamba Ibn Mas'ud amesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Maisha hayatomalizika wala hayatokwisha mpaka mtu atakaetokana na kizazi changu, mwenye jina kama langu, atakapotawala."*

Kwahiyo, al-Mahdi atatokamana na kizazi cha Mtume (صلى الله عليه وسلم), na jina lake litakuwa ni Muhammad Bin Abdullaah. Lakini hatahivyo, haikubainika wazi iwapo atakuwa ni kwenye kizazi cha al-Hasan au al-Husein. Hii ni kwa sababu riwaya zote zenye kutaja mas'ala haya ni dha'eef. Amependekeza *Sheikh ul Islaam*, Ibn

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Taymiyyah yakwamba al-Mahdi atakuwa ni katika kizazi cha al-Hasan Ibn Ali, kwa sababu ameikubali kauli iliyonasibishwa na Ali Ibn Abi Twaalib. Lakini hatahivyo, Sheikh Muhammad Naasir ud Deen al-Albaani ameidhoofisha riwaya hii kwenye kitabu chake ***Mishkaat-ul-Masaabih.*** Ama kuhusu umbile lake, amepokea Abu Sa'eed yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema kama ilivyopokewa kwa njia ya sawa na Abu Daawud na al-Haakim: *"Al-Mahdi atakuja kutokamana na mimi (kizazi changu). Atakuwa na komo (bapa lake la uso) pana na pua yake itakuwa ndefu, nyembamba yenye ncha. Ataeneza uadilifu na usawa baada ya kuwa na dhulma na maonevu. Atatawala kwa muda wa miaka saba."*
Hadeeth hii imebainisha yakwamba utawala wa al-Mahdi utadumu kwa miaka saba.
Vilevile Abu Sa'eed al-Khudhree amepokea yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Ulimwengu utajaa dhulma na maonevu. Utakapokuwa na dhulma na maonevu mengi, Allaah atamuinua mtu anaetokamana na kizazi changu, jina lake litakuwa kama jina langu na jina la babake litakuwa ni kama jina la babangu. Ataujaza (ulimwengu) uadilifu na usawa. Ataishi na nyinyi kwa muda wa miaka saba au minane. Ikiwa ataishi zaidi ya hapo, basi itakuwa miaka tisa." Atakapokuja kwa mara ya pili, 'Issa (عليه السلام) ataswali nyuma ya al-Mahdi.* Bukhari na Muslim wamepokea yakwamba amesema (صلى الله عليه وسلم): *"Mutakuwaje pindi mwana wa Maryam atakapowateremkia?"*
Vilevile Abu Na'im amepokea *sanad* iliyo swaheeh mpaka kwa Abu Sa'eed inayosema yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Miongoni mwetu ni yule ambaye 'Issa mwana wa Maryam ataswali nyuma yake."*
Imaam Muslim amepokea yakwamba Jaabir bin Abdullaah amesema yakwamba alimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: *"Kundi la Taifa langu litapigana haliyakuwa limeshikamana na haki wabakie kuwa ni washindi mpaka siku ya Malipo."*
Kisha akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم), *"Kisha atashuka 'Issa mwana wa Maryam. Kiongozi wao atasema, 'Njoo utuswalishe.' Atasema, 'Laa. Baadhi yenu ni viongozi wa wengine wenu kama heshima itokayo kwa Allaah juu ya Taifa hili.'"*
Sisi tunaamini yakwamba ahaadeeth zifuatazo zinamuhusu al-Mahdi; *"Miongoni mwa mwisho wa Taifa langu, kutakuwepo na Khalifa atakaejitolea kwa kuteka hundi la pesa kwa mkono wake bila ya kuzihesabu."* Hii ni sehemu ya hadeeth ambayo Imaam Muslim aliyoipokea katika swaheeh yake. Katika riwaya nyengine ya hadeeth hii, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Miongoni mwa ma-Khalifa wenu, patakuwepo na khalifa ambaye atakaejitolea kwa kuteka hundi la pesa kwa mkono wake bila ya kuzihesabu."*
Huduma ya ahaadeeth hizi ni kuonyesha yakwamba kutakuwa na vita vingi baina ya Waislamu na maadui zao. Vilevile, hadeeth hizi zinaonyesha yakwamba ushindi wa Waislamu dhidi ya makafiri na kama matokeo yake, mali ya nyara, zitakuwa nyingi wakati huo.
Ama kuhusu kutokeza kwa al-Mahdi, hayo yatatokea baada ya Allaah kumtayarisha kuongoza Taifa hili, kama alivyosema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Al-Mahdi ni miongoni mwetu, Ahlu al-Bayt (Jamii ya* Mtume (صلى الله عليه وسلم)*). Allaah atamtayarisha (kwa kazi ya uongozi) kwa usiku mmoja."*
Hadeeth hii yamaanisha yakwamba Allaah atamtayarisha al-Mahdi kuongoza Taifa hili kwa usiku mmoja, na Allaah ni Mwenye 'Ilmu iliyokamilika. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimueleza al-Mahdi kama mtu mwema, akasema: *"Na Imaam wao atakuwa ni mtu mwema."*
Baada ya Allaah (سبحانه وتعالى) kumtayarisha al-Mahdi kwa uongozi, viongozi wa zama hizo watajaribu kumuuwa. Al-Mahdi atakimbia na atahamia mafichoni Makkah, pamoja na wafuasi wake, wakiwa madhaifu, si kwa idadi wala silaha. Kutatumwa jeshi kuja kumuuwa. Haya yameelezwa na Imaam Muslim alipopokea yakwamba Umm Salamah amesema: "Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم), "Mkimbizi atatafuta hifadha katika *al-Bayt* (msikiti mkubwa wa Makkah). Kutatumwa jeshi kwenda kumshika mpaka lifike *al-Baydhaa'* [Msikiti Mkubwa wa Makkah, - *hapa ni mahali penye ardhi iliyotandazika iliyoko pambizoni mwa Mji wa Madinah kuelekea sehemu ya kusini, kwenye barabara ya kuelekea Makkah].* Mahali ambapo ardhi itakapo poromoka chini yao.' Nikasema, Yaa Rasoolullaah! Je kwa yule ambaye aliyekuwa hapendelei (kuwa na jeshi hilo)?' Akasema, 'Ardhi itaporomoka chini yao, lakini atafufuliwa siku ya Malipo kulingana na niya yake ya ki-hakika.'"
Pia amepokea Imaam Muslim yakwamba Hafswah alimsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: *"Jeshi la uvamizi litaelekea al-Bayt* [Msikiti Mkuu wa Makka]. Watakapofika *al-Baydhaa'*, ardhi itaporomoka chini ya safu za kati za jeshi lao. Jeshi lao lililo katika safu za mbele litawaita walio kwenye safu za nyuma. Kisha ardhi itaporomoka chini yao. Hapana atakaenusurika isipokuwa baadhi ya majeruhi watakaosimulia kuhusu mkasa huo."
Katika riwaya nyengine ya hadeeth hii, Hafswah amepokewa akisema yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Pote la wakimbizi, lisilokuwa na jeshi imara kulingana na idadi yao au silaha watakimbilia kwenye Nyumba hii* [Msikiti Mkuu wa Makka] na jeshi litatumwa kuwashika. Watakapofika *al-Baydhaa', ardhi iliyo chini yao itaporomoka."*
Vilevile Imaam Muslim amepokea kutoka kwa 'Aaisha (رضي الله عنها) yakuwa amesema: "(Siku moja) Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akibabaika akiwa kwenye usingizi. Tukasema, 'Yaa Rasoolullaah! Ulifanya mambo fulani kwenye usingizi wako ambayo hatujawahi kukuona ukiyafanya hapo awali.' Akasema, *'Ndio, ni jambo la kushangaza mno, ukweli ni kwamba baadhi ya Taifa langu litaelekea kwenye al-Bayt, ambapo mtu mmoja kutoka katika kabila la Quraysh atakimbilia kujificha ndani ya Nyumba. Pindi watakapofika al-Baydhaa', ardhi itaporomoka chini yao.'* Tukasema, 'Yaa Rasoolullaah! Hiyo njia si itakuwa imewakusanya watu tafauti.' Akasema, *'Na'am, ni kweli. Baadhi yao watakuwa ni wenye kutafuta njia (ya kuelekea Makkah), kutakuwa na wale waliolazimishwa, na wasafiri. Lakini hatahivyo, wote wataangamia na watafufuliwa mbalimbali, kwani Allaah atawafufua kulingana na niya zao.'"*
Pia Umm Salamah amesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Kundi la Taifa langu litaangamia kutokana na kuporomoka kwa ardhi. Watatumilizwa kwenda (kumuuwa) mtu atakaekuja Makkah, lakini Allaah atamuhifadhi na vitimbi vyao. Ardhi itaporomoka chini yao. Hata hivyo, wote wataangamia pamoja, watafufuliwa wakiwa mbalimbali kwa sababu baadhi yao watachukizwa (na kwenda kumuuwa al-Mahdi), lakini watalazimishwa kujiunga nao (jeshi)."*
Vilevile mkewe al-Qa'qaa' bin Abi Hadrad al-Aslami amesema yakwamba amemsikiya Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: *"Enyi watu! Pindi mutakaposikiya kulihusu jeshi*

(Continued from page 3)

litakaloangamia kwa maporomoko ya ardhi hapa karibu yetu, basi mujue yakwamba Kiyama kimekurubia."

Hadeeth hizi zinaeleza yakwamba jeshi litatumilizwa kwenda kumuuwa al-Mahdi, ambaye atakaejificha kwenye Nyumba pamoja na baadhi ya waumini watakaomfuata. Jeshi hili litaangamia lifikapo *al-Baydhaa'* , ardhi iliyotandazika pambizoni mwa Madinah ikiwa imeelekea Makkah. Baadae, al-Mahdi atapewa *Bay'ah* kama Khalifa wa Waislamu. Atawaongoza Waislamu kwenye vita vyingi vya *Jihaad*. Utawala wake utakuwa ni Ukhalifa utakaofuata uongofu wa Mtume na vita vyingi vitatokana baina ya Waislamu na makafiri katika wakati wake, mpaka Allaah atakapomteremsha 'Issa, mwana wa Maryam (عليه السلام). Ni katika zama za al-Mahdi ambapo ushindi wa pili wa Constantinople (Istanbul) utakapotokea, muda mchache kabla ya kutokeza kwa al-Maseeh ad-Dajjaal na kuja kwa mara ya pili kwa 'Issa (عليه السلام).

Amesema Yusayr bin Jabir, "Dhoruba la mchanga mwekundu litafoka katika mji wa al-Kufah. Kisha, atakuja mtu na huku akipiga makelele na kuyarudia rudia maneno yake, 'Yaa Abdullaah bin Mas'ud! Kiyama kishakuja." Kisha, (Yusayr) akasema yakwamba aliketi baada ya kuwa ametegemea (katika upande wake) na akasema, 'Kiyama hakitokuja mpaka pakosekane urathi utakaogawanywa na pasipatikane ngawira zitakazoleta utoshelezaji (kwa sababu ya majeruhi wengi).' Akaashiriya kwa mkono wake kuelekea ash-Shaam na huku akisema, 'Maadui watakusanya jeshi lao dhidi ya wafuasi wa Uislamu.' Nikasema, 'Unamaanisha ar-Rum?' Akasema, 'Na'am. Kisha, wakati wa vita hivyo, kutakuwa na mashambulizi makali.Waislamu wataomba wasaidizi wa kijeshi watakaojitolea kufa au warudi wakiwa ni washindi. Watapigana mpaka usiku uwagawanye miongoni mwao. Sehemu zote mbili zitarudi kwenye kambi zao haliyakuwa si washindi na vita hivyo vitatokomea. Kisha Waislamu (katika siku ya pili) wataomba wasaidizi wa kijeshi watakaojitolea kufa au warudi wakiwa ni washindi. Watapigana mpaka usiku uwagawanye miongoni mwao. Sehemu zote mbili zitarudi kwenye kambi zao haliyakuwa si washindi na vita hivyo vitatokomea. Kisha (katika siku ya tatu) Waislamu wataomba wasaidizi wa kijeshi watakaojitolea kufa au warudi wakiwa ni washindi. Watapigana mpaka usiku uwagawanye miongoni mwao. Sehemu zote mbili zitarudi kwenye kambi zao haliyakuwa si washindi na vita hivyo vitatokomea. Katika siku ya nne, jeshi lote la Waislamu watasimama dhidi yao (makafiri) na Allaah atawashinda (makafiri). Watapata majeruhi wengi ambao hawajawahi kupata mfano wake hapo awali ...' au alisema, 'Hawajawahi kuonekana hapo awali, hata ndege watakaoruka karibu yao hawatowapita bila ya kuanguka wakiwa wamekufa. Baadae, vijana wa baba mmoja (kutoka upande wa Waislamu), waliokurubia mia moja, watawahesabu majeruhi na watakuta yakwamba aliyepona ni mmoja tu. Kwahivyo, watatosheka vipi na mali hiyo ya nyara na urathi utagawiwa vipi hapo? Watakapokuwa wanafanya hayo, watasikiya mkasa mkubwa zaidi kuliko huo; nao ni kwamba, mtu atapiga makelele miongoni mwao akisema yakwamba ad-Dajjaal ametokeza miongoni mwa jamii zao waliowaacha huko nyuma. Watatupilia mbali waliyokuwa wameyashika kwa mikono yao na waelekee huko. Watapeleka watu kumi na Farasi wao kama jeshi la kupigana. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: *"Mimi nawajua majina yao na majina ya baba zao na rangi za Farasi wao. Hao ndiwo watakaokuwa ni wapelekaji Farasi walio bora katika ulimwengu mzima,'* au alisema, '*(Wao) watakuwa ni miongoni mwa wapelekaji Farasi walio bora ulimwenguni.'"*

Vilevile, Abu Hurairah amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Qiyama hakitotokea mpaka kambi ya ar-Rum itakayokuwa al-Aa'maq au Dabiq. Kisha, jeshi litokalo Madinah, miongoni mwa watu wema zaidi ulimwenguni katika siku hizo, wataelekea huko. Kambi hizo mbili zitakapokutana, ar-Rum watasema, hebu tupiteni kwa wale waliowashika baadhi yetu, ili tupigane nao.' Waislamu watasema, 'Laa, Wallaahi! Hatutowaacha kupita kwenda kwa ndugu zetu.' Watawapiga na thuluthi moja (ya Jeshi la Waislamu) watakimbia, nao ni wale ambao Allaah hatowasamehe. Thuluthi nyengine watauwawa wakiwa mashahidi, nao watakuwa ni mashahidi walio bora mbele ya Allaah. Thuluthi (ya mwisho) ndio watakaokuwa ni washindi na hawatoingia kwenye fitnah. Watawapiga na kuwashinda Constantinople (Istanbul). Kisha watakapokuwa wakigawanya mali ya nyara na kuyaangika mapanga yao kwenye miti ya Zaytuni, Sheytwaan atapiga mayoe baina yao, 'Maseeh (mrongo) ameshatokeza miongoni mwa jamii zenu.' Wataregea makwao kwenda kupambana nae. Ingawaje, mshtuko huo au habari hizo ni za urongo, watakapofika ash-Shaam, atatokeza. Watakapokuwa wakijitayarisha kupigana, wakistawisha mistari yao, swala italinganiwa (iqaamah) na 'Issa mwana wa Maryam, atashuka awe ni kiongozi wao. Pindi adui wa Allaah (ad-Dajjaal) atakapomuona, atayayuka, kama ambavyo chumvi inavyoyayuka kwenye maji. Kama angeliwachwa peke yake, angeliyayuka mpaka amalizike. Lakini hatahivyo, Allaah atamuuwa kwa ('Issa) Mkono Wake na atawaonyesha (Waislamu) damu yake kwenye mkuki wake.'"*

Hadeeth hii inaeleza yakwamba 'Issa ataongoza Taifa la Waislamu. Katika riwaya nyengine ya hadeeth hii, Muslim amepokea yakwamba Abu Hurairah amesema: *"Na yeye ('Issa) atawaongoza nyinyi kwa Kitaab cha Mola wenu (Al-Qur'an) na Sunnah za Mtume wenu* (صلى الله عليه وسلم)."

Riwaya hii inaonyesha waziwazi yakwamba 'Issa atawaongoza Waislamu kwa Qur'an na Sunnah na wala sio kwa Sheriya aliyowapelekea wana wa Israel. Kabla ya vita vya ar-Rum na Waislamu kutokea. Patakuwa na makubaliano ya kusimamisha vita baina yao. Kisha, ar-Rum watavunja makubaliano hayo kwa kufanya udanganyifu wakaja kupambana na Waislamu kwa vipote thamanini, kila kipote kikiwa na wanajeshi Elfu kumi, na katika riwaya nyengine "... Elfu kumi na mbili." Hapo ndipo pale al-Malhamah itakapoanza na ndipo pale Waislamu watakapowashinda wa-Rumi. Amepokea Abu Daawud yakwamba mmojawapo wa Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Mutashirikiana katika kupanga mkataba pamoja na wa-Rumi na mushirikiane nao katika kupigana na adui nyuma yenu. Nyote (wawili) mutakuwa ni washindi na mutagawanya mali ya nyara na mutakuwa na usalama. Mutarudi kwenye mapumziko katika kambi ya Marj Dhi Tuloul. Kisha mkristo atauinua msalaba na apige mayoe, 'Msalaba umeshinda vita.'* Muislamu atakasirika na atamuuwa. Hapo ndipo pale ar-Rum watakapo onyesha udanganyifu wao wajiandae kwenda *al-Malhamah.'"*

[ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO]